

**KUTABIRIWA MTUME
WA UISLAMU NDANI
YA VITABU VYA
KIHINDU, KIKIRISTO,
KIYAHUDI NA KIPARSI**

Kimeandikwa na:

Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi

Kimetafsiriwa na:

Sheikh Jamal Abdalla

Kimetolewa na Kuchapishwa na:

Bilal Muslim Mission of Tanzania

P.O. Box 20033,

Dar es Salaam

TANZANIA

**KUTABIRIWA MTUME WA
UISLAMU NDANI
YA VITABU VYA
KIHINDU, KIKRISTO,
KIYAHUDI NA KIPARSI**

Kimeandikwa na:

Sayyid Saeed Akhtar Rizvi

Kimetafsiriwa na:

Sheikh Jamal Abdalla

**Kimetolewa na Kuchapishwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania**

**S.L.P. 20033
Dar es Salaam, Tanzania**

Haki za kunakili imehifadhiwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania



ISBN: 9987 620 20 5

Toleo la Kwanza:
Muharram, 1425 / March, 2004
Idadi:
Nakala 2,000

Kimetolewa na Kuchapishwa na:
BILAL MUSLIM MISSION OF TANZANIA
S.L.P 20033
DAR ES SALAAM
TANZANIA

YALIYOMO

1. Utangulizi	2
2. Dibaji	4
3. Kutabiriwa Mtume (s.a.w.w.)	5
4. Barm Uttar Khand	7
5. Kalki Puran	10
6. Kutoka Kalki Avatar	13
7. Kutoka Atharva Ved	15
8. Agano la Kale na Agano Jipya	16
9. Kitabu cha Mwanzo	16
10. Kumbukumbu la Tawrati	17
11. Tabiri nyinginezo	20
12. Ndani ya Agano Jipya	22
13. Vitabu vya Kiparsi (Umajusi)	25

**KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU,
MWINGI WA REHEMA,
MWENYE KUREHEMU**

**Shukurani zote ni Zake Mwenyezi Mungu;
Mola wa walimwengu wote; Mwingi wa
Rehema, Mwenye kurehemu; Mfalme pekee
siku ya malipo; Wewe tu ndiye
tunayekuabudu, na Wewe tu ndiye
tunayekutaka msaada; utuongoze katika
njia iliyonyooka; njia ya wale Ulio
waneemesha,
sio ya wale Uliowakasirikia, wala ya wale
waliopotea.**

**Ewe Mwenyezi Mungu! Mshushie Rehema
zako Bwana wa Mitume Wako, na wa
mwisho wa Manabii Wako Muhammad - na
kizazi chake Kitoharifu na kilichosafishwa.
Pia washushie Rehema Zako Mitume wote
na Maimamu.**

UTANGULIZI

Tunamshukuru Allah (s.w.t.), kwa Baraka za Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) na Watukufu Ahlul-Bait (a.s.) kwa kutujaalia kuweza kufanikisha juhudi zetu hizi katika kuchapisha kitabu hiki “***Kutabiriwa Mtume Wa Uislamu Ndani Ya Vitabu Vya Ki-Hindu, Ki-Kiristo, Ki-Yahudi na Ki-Parsi?***”.

Kitabu kilichopo mikononi mwako ni tafsiri ya moja ya maandishi ya Allamah Sayyid Saeed Akhtar Rizvi (r.a.). Kitabu hiki kimekuwa maarufu katika ulimwengu wa Ki-Islamu na kilitafsiriwa na kuchapishwa na taasisi mbali mbali kwa lugha ya Ki-Ingereza, Ki-Farsi, Ki-Hindi na Ki-Gujrati.

Sababu iliyoifanya Bilal Muslim Mission isimamie kazi hii ni kama zile za mwanzo, ambayo inatokana na maombi ya watu wengi kutoka Afrika ya Mashriki kututaka tuchapishe Kitabu hiki kwa lugha ya Ki-Swahili. Hii ilitufanya tutafsiri na kuchapish kitabu hiki ili watu wazungumzao kiswahili wa weze kuelewa na kufahamu zaidi.

Mimi binafsi sikusita kumuomba ndugu yetu Sheikh Jamal Abdallah kukitafsiri kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili kutoka kwenye asili yake ya lugha ya Ki-ingereza, na Al-Haj Dr. Muhammad Kanju ameipitia tarjuma hii na kuisahihisha. Nawashukuru Sheikh

Jamal na Dr. Kanju kwa kukubali ombi langu na kuifanya kazi hii kwa moyo mmoja,

Bilal Muslim Mission inatoa shukurani zake za dhiti kwa wale wote ambao kwa juhudi zao kitabu hiki kinawafikia wasomaji wetu mikononi mwao na wale wote wanaotuunga mkono kwa njia moja au nyingine katika kazi zetu za Tabligh. Tunamuomba Allah (s.w.t.) awalipe malipo mema hapa Duniani na baadaye huko, Akhera.

13th February, 2004
Dar es Salaam

Sayyid Murtaza Rizvi
Bilal Muslim Mission

DIBAJI

Utabiri huu ulichapishwa mara ya kwanza kama sehemu ya kitabu *Prophethood* (Utume), mwaka 1970, na Bilal Muslim Mission of Tanzania, Dar-es-Salaam.

Tokea wakati huo, kilichapishwa mara nyingi - Dar-es-Salaam na Mombasa.

Kisha taasisi ya “Word Islamic Network” (WIN) ya Bombay, ilichapisha sehemu hii kama kijitabu kinacho jitegemea, chini ya anuani, *Prophecies About The Holy Prophet of Islam in Hindu, Christian & Jewish Scripture*”. (Kutabiriwa Mtume wa Uislamu ndani ya vitabu vya Kihindu, Kikristo na Kiyahudi).

Sasa Bilal Muslim Mission inapenda kukichapisha tena, na nimezipitia upya taarifa zote kwa ajili ya toleo hili, na kuongeza utabiri kutoka katika vitabu vya Kiparsi - nataraji kitakuwa maarufu kuliko hapo awali.

Wa Billahi't-tawfiq

Sayyid Saeed Akhtar Rizvi

11th Shawwal, 1422 / 27th Desemba, 2001

Dar-es-Salaam

KUTABIRIWA MTUME MTUKUFU

Kwa kuwa Mtume Mtukufu wa Uislamu angeleta dini ya Ulimwengu mzima kwa ajili ya binadamu, na kwa kuwa dini hiyo ilibidi iendelee hadi mwisho wa dunia, Manabii wote katika dini zote za duniani waliwafahamisha wafuasi wao kuja kwake, na wakawaamrisha kuifuata dini yake bila kipingamizi chochote.

Sehemu nyingi waliwaeleza habari za maisha yake binafsi na ya familia yake ili watu waweze kuwatambua kwa urahisi.

Si rahisi kueleza katika kijitabu hiki kidogo utabiri wote kutoka ndani ya vitabu vyote. Hata hivyo, nakusudia kutoa hapa utabiri mchache kutoka ndani ya vitabu vya kidini vya Wafursi, Wahindu, Wayahudi na Wakristo.

Ni muhimu kutaja kwamba katika sehemu nyingi, habari njema zinazomhusu Mtume Mtukufu wa Uislamu hufuatiwa na maelezo ya watu wa familia yake ambao watakuwa washika makamo wake. Nimetoa baadhi ya utabiri huo. Vitabu vingi muhimu vimeandikwa kuhusu mada hiyo katika karne iliyopita. Miongoni mwa vitabu hivyo muhimu ni:

1. **Mir'ātu 'l-Makhlýqāt**, cha marehemu Molvi Abdu'r-Rahman Chishti wa India. Kitabu hiki

kiliandikwa katika mwaka 1041 wa Hijriya (= 1631-32 A.D.). Kina tafsiri za sehemu muhimu za vitabu vitakatifu vya kihindu.

2. **Bashārat-e-Ahmadi**, cha marehemu Molvi Abdul-Aziz, wa Lucknow.
3. **Anisu ‘I-a‘laam**, cha marehemu Fakhul-Islam Muhammad Sadiq. Alikuwa ni muarmenia ambaye hapo kabla alikuwa ni padri wa Kikristo. Alikifahamu Kilatini, Kiyunani, Kiebrania, Kisinia, Kiarmenia, Kiajemi na Kiarabu. Aliukubali Uislamu kutokana na utafiti wake kuhusu maana ya neno ‘*Paracletos*’ ambaye kuja kwake kumetabiriwa katika *Injili* ya *Yohana*. Aliamini kwamba neno hilo lilimhusu Mtume Muhammad (s.a.w.w.).

Kitabu chake katika juzuu mbili, kwa Kiajemi, kilichapishwa mwaka 1891 A.D. Kitabu hicho ni hazina kubwa ya utafiti kwa wale wote ambao wana shauku katika ulinganishaji wa dini; na karibu vitabu vyote vilivyoandikwa baadaye vinategemea kitabu hicho (ingawa ni watu wachache waliokiri jambo hilo).

Utabiri wa kifursi zimechukuliwa kutoka utabiri wa Zoroasta uliomo ndani ya (vitabu viitwacho) *Zend Aresta* na *Dasatir*, kama ilinukuliwa ndani ya kitabu cha A. H. Vidyarthi & U. Ali, (kiitwacho) “Muhammad in Parsi, Hindu and Buddhist Scriptures” (*Muhammad ndani ya vitabu vya kifarsi, kihindu na kibudha*).

Utabiri unaotolewa hapa zimechukuliwa kutoka vitabu hivi.

BARM UTTAR KHAND

Barm Uttar Khand ni kitabu cha dini ya kihindu. Marehemu Abdur-Rahman Chisti (wa karne ya 11 ya Hijriya) alikitafsiri kwa kiurdu ndani ya kitabu chake “*Mir’ātu ’l-Makhlýqât*”. Kwa mujibu wa kitabu hicho, avatar mashuhuri wa kihindu, Mahadev alimuambia mkewe, Parbati, matukio yote ya baadae, walipokuwa mlimani, Kailash Parbat, na mfuasi wake Bishist Muni akayandika (maneno hayo). Sehemu husika imetafsiriwa hapa kutoka ndani ya *Muqaddamah Anwāru ’l Qur ’ān* (cha marehemu Maulana Sayyid Rahat Husain Gopalpuri) Uk. 40-43.

Mahadevji anasema:-

Baada ya miaka elfu sita, Mwenyezi Mungu Mtukufu atamuumba mtu wa maajabu miongoni mwa wana wa Adam huko Mundarne, iliyo baina ya bahari (nyingi)¹...
... Ewe Parbati, atatokana ndani ya mgongo wa *Kant Bunjh*;² naye (Abdullah) atakuwa na uchamungu na ujuzi wa Mungu mfano wa mto; hivyo (kutoka ndani ya mto huo) itachomoza lulu. Na jina la mkewe litakuwa ‘*Sank*

1 Bara Arabu imezunguukwa na bahari pande zake tatu.

2 ‘Kant Bunjh’ maana yake ‘Mtumishi wa Mungu’ ambapo kwa Kiarabu inakuwa “Abdullah”. Abdullah lilikuwa jina la baba yake Mtukufu Mtume.

Rakhiya'³ Naye (yaani Abdullah) atakuwa amesoma vitabu vitatu; na atakiacha kitabu cha nne baada ya kusoma tu: “Alif Lam Mim”... .. Ewe Parbati, yeye (yaani Abdullah) atakua ni chifu ndani ya kabila lake; watu kutoka vijiji vyote watakuwa mlangoni kwake na watamfuata. (Mtoto wa Abdullah) hatawaogopa viumbe; atakua shujaa sana na mwenye elimu ya Allah, na jina lake litakua ‘MAHAMAT’. Watu watashangazwa kuona mfumo wake... .. Hatoabudu kama watakvoyokuwa wakiabudu watu wa kabila lake na atawaambia watu wake kwamba “Nmeambiwa na yule Mwenye nguvu na (Mungu) wa Pekee nisijiingize ndani ya ibada zisizo na maana; na mimi sielekei ila kwa Allah hivyo yapasa mnifuate.”⁴ Ewe Parbati, Mahamat atafundisha sheria yake binafsi kwa viumbe wote, kwa kufuta njia zote za kuabudu na sheria zilizopita; na atajaribu kuwafanya watu wote wamfuate. Hatua kwa hatua, watu wasio idadi wataingia katika dini yake na wengi wao watamfikia Mungu.

Na kama watu wanavyotumia zama yetu ya *Sakh*, hivyo hadi mwishoni mwa Kaljug (zana za mwisho) watu wataona zama za MAHAMAT.⁵... Ewe Parbati baada

3 ‘Sank Rakhiya’ maana yake ‘Amani’ ambapo kwa Kiarabu ni “Amina”; Jina la mama yake Mtukufu Mtume.

4 Linganisha na Aya ya Qur’ani:

“Sema: Nimeamrisha kumwabudu Mwenyeezi Mungu tu wala nisimshirikishe, kuendea kwake ndio ninaita na kwake ni marejeo yangu.”(13:36)

5 Yaani zama za Hijira

yake (baada ya kifo cha mtoto wa Muhammad wa kiume) Mwenye nguvu zote ambaye mfano Wake hakuna, atampa Mahamat binti⁶ ambaye atakuwa ni bora kuliko wavulana 1000, na atakua mzuri sana asiye na mfano, na mkamilifu sana katika kumuabudu Mungu. Kamwe hatafanya kosa lolote; atakuwa amehifadhiwa kutokana na kila dhambi - ndogo au kubwa; na kwa kupitia kwa baba yake atakuwa karibu sana na Mungu. Hivyo Mwenye nguvu (Mungu) atampa binti ya Mahamat watoto wawili (wa kiume)⁷, wote wawili watakua ni wenye kupendeza na wenye kupendwa na Mungu, wenye nguvu, wenye elimu ya Mungu, majasiri, mashujaa na wasio na mfano katika matendo mema. Na Mwenye nguvu (Mwenyezi Mungu) hatoumba baada yao binadamu yoyote akiwa na ukamiifu wa aina hiyo katika mema yaliyojificha na yaliyo wazi.

Hao hao watoto wawili wa Mahamat watakuwa washika makamo wake (warithi); na watakuwa na watoto wengi na watawaleta watu katika dini ya Mahamat siku hadi siku kwa hoja zao za kweli; na wataiangazia dini ya Mahamat. Na Mahamat atawapenda kuliko watu wake wote, hata zaidi ya binti yake mwenyewe. Na vijana hawa wawili watakuwa wakamilifu katika dini ya Mahamat; hawatofanya kazi yoyote kwa ajili ya matamania yao binafsi, na kauli na matendo yao yote yatakuwa kwa ajili ya ridhaa ya Mwenyezi Mungu.

Ewe Parbat, miaka michache baada ya kifo cha

6 'Fatimah', Bibi wa Peponi, Chifu wa wanawake wote.

7 Imamu Hasan (a.s.) na Imamu Husein (a.s.)

Mahamat, baadhi ya watu wabaya watawauwa hawa wajukuu wa Mahamat bila sababu yoyote; kwa ajili tu ya tamaa za dunia; dunia nzima itakuwa “bila kichwa” kwa vifo vyao (hawa vijana wawili). Wauwaji wao watakuwa ni “*Maliksh*” (Mlahidi, mtu asiyesadiki kuwa yupo Mungu), waliolaaniwa duniani na akhera; hawatakuwa na mapenzi juu ya Mahamat na hawatapata wokovu kutokana na ‘*Nark*’ (yaani jehanamu). Lakini kwa muonekano watakuwa katika dini ya Mahamat, na pole pole wengine watawafuata, kwa kiburi watafanya mambo mengi kinyume na njia ya Mahamat na wanawe. Watu wachache tu ndio watakaobaki katika njia ya Mahamat. Wengi watafuata njia ya wale walioua watoto wa Mahamat; na bado katika muonekano, wataitwa wafuasi wa Mahamat; na siku za mwisho ya *Kaljug* (zama za mwisho) watakuwepo wengi miongoni mwa wanafiki hao na watasababisha vurugu katika dunia nzima”.

Baada ya hapo Mahadevji anelezea kudhihiri kwa Imam Mahdi; kutokea Qiyamah na kuingia Peponi kwa Bibi Fatimah pamoja na wafuasi wake.

KALKI PURAN

Katika vitabu vingi vya wahindu, kumetajwa kutokeza ma ‘Avatar’ kumi. Tisa wamekwisha kuja na wa kumi anangojewa na wahindu. Jina alilopewa huyu Avatar wa kumi ni “*Kalki Avatar*” (Mtume Kalki). Maelezo na dalili, zinazopatikana ndani ya vitabu zinakubaliana

moja kwa moja na zile za Muhammad Mustafa (s.a.w.w.).

Kalki Puran ni moja wapo wa vitabu vitakatifu vya wahindu. Imeandikwa ndani ya kitabu hiki kwamba sababu ya Nabii huyu kufahamika kama “Kalki Avatar”, ni kuwa ataondoa Kalki (kutu na giza) kutoka katika mioyo ya watu, na atashinda vitimbi vyote vya watu wabaya.

Imeandikwa pia kuwa watu wa jumuiya yake watakuwa ni wenye kumuabudu Mungu.

Jina la baba yake Nabii Kalki ni “Vishunais” mchanganyiko wa maneno mawili, *Vishnu* (mungu) na *ais* (mja): yakiwekwa pamoja yanamaanisha “mja wa Mwenyezi Mungu”. Hii ni maana ya Abdullah, jina la baba yake Muhammad Mustafa (s.a.w.w.).

Jina la mama yake Nabii Kalki ni “Somti” linalomaanisha “Muaminifu”. Na jina la mama yake Mtume Muhammad (s.a.w.w.) lilikuwa Amina, ambalo pia linamaanisha “Muaminifu”.

Imeandikwa pia kuwa Nabii Kalki atakuwa na ndugu watatu waitwao Kavi, Samati, na Parak.

1. “Kavi” maana yake ni “mwenye hekima” na hiyo hiyo ni maana ya ‘Aqeel’.

2. “Samati” maana yake ni ‘Ujuzi’ na hiyo hiyo ni maana ya ‘Ja’far’
3. “Parak” maana yake ni “Aliye katika nafasi ya juu” na hiyo hiyo ni maana ya ‘Ali’.

Aqeel, Ja’far na Ali walikuwa ni (binamu) ndugu watatu wa Mtume Muhammad Mustafa (s.a.w.w.).

Sehemu ya kuzaliwa Nabii Kalki imeelezwa kuwa ni “Shambhal Nagari” - jina lililopewa nchi ya Hijaz uarabuni. “Shambhal” maana yake ni “mchanga” na “Shambhal Nagari” maana yake ni nchi ya mchanga au “jangwa” ambalo linakubaliana vema na kisanga cha Uarabuni (Arabian Peninsula).

Kuhusu Nabii Kalki, imeandikwa pia kuwa ataabudu pangoni. Inafahamika vema katika Ulimwengu wa ki-Islamu kuwa Muhammad Mustafa (s.a.w.w.) alipata “Wahyi” wake wa kwanza katika Pango la mlima Hira - kijimlima cha jangwani na sehemu yake aliyoichagua ya kuwa faragha karibu na Makka.

Pia katika “Kalki Puran”, imeandikwa kuwa atapata elimu kupitia kwa “Prash Ram” maneno yanayomaanisha “Roho wa Mungu”. Inafahamika vema na Waislamu wote kuwa ni malaika Jibril ndiye aliyeleta “Wahyi” wa kwanza kwa Muhammad Mustafa (s.a.w.w.) katika pango la mlima Hira. Jibril anaitwa “Ar-Ruh-al-Amin” (Roho Mwaminifu) katika Uislamu.

Kisha imeandikwa kwamba Nabii Kalki atamuowa binti wa mfalme wa Shambhal Deep. Hivyo Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alimuoia mwanamke tajiri zaidi uarabuni, aliyeitwa Khadija.

Imeandikwa pia kwamba Nabii Kalki atahama kuelekea vilima vya kaskazini. Hivyo kwa amri ya Mwenyezi Mungu, Mtume Muhammad Mustafa (s.a.w.w.) ilimbidi ahame kutoka Makka kwenda Madina ambayo ipo kaskazini.

KUTOKA KALKI AVATAR

Miaka 17 baada ya kutokeza kwa kitabu changu mwaka 1970, Pandit Vedaprakash Upadhyai, Brahmin wa ki-Bengali aliyekuwa katika chuo kikuu cha Allahabad, alichapisha kitabu chake *Kalki Avatar*. Ndani ya kitabu hicho alishuhudia ya kwamba maelezo ya kiongozi “anayesubiriwa” na kiongozi Kalki Avatar, yanakubaliana na Mtume Muhammad wa Uarabuni peke yake. Maoni yake yalithibitishwa na ma ‘Pandit’ wengine wanane wakubwa.

Alizitaja ‘Puran’ na akatoa tafsiri yake; Tunatoa hapa kiini cha maelezo yake:-

1. Kalki Avatar atakuwa ni Mjumbe wa mwisho wa Mungu, na atadhihiri kwa ajili ya kuuongoza Ulimwengu mzima. (Sifa hii inajieleza wenyewe).

2. Atazaliwa kisiwani (Arabuni imezungukwa na bahari katika pande zake tatu)
3. Jina la baba yake ni Vishnubhagat. (Vishnu = Mungu; Bhagat = Mja au Mtumwa; Vishnubagat = Mtumwa wa Mungu = ‘Abdullah’).
4. Jina la mama yake ni Sumaani. (Sumaani = Amani = Aminah).
5. Chakula chake cha asili kitakuwa tende na zaituni (Na ndivyo ilvyokuwa)
6. Atakuwa ni mtu mnyofu mno na mkweli sana. (As-Sadiq al-Amin = sifa maarufu za Mtume (s.a.w.w.).)
7. Atazaliwa ndani ya ukoo wenye heshima (Quraish na hasa Bani Hashim zilikuwa ni kabila na koo zenye kuheshimika sana).
8. Mwenyezi Mungu atamfundisha kupitia kwa Mjumbe Wake ndani ya Pango. (Wahyi wa kwanza uliletwa kwake na Jibra’il katika Pango la Hira).
9. Mwenyezi Mungu atampa farasi aendae kasi ili asafiri duniani kote na mbinguni (Inaelezea Buraq na Kupaa Mi’raj)
10. Atakuwa ni mpanda farasi na mpiganaji bora (Haina haja ya maelezo zaidi).

KUTOKA ATHARVA VED

Marehemu Molvi Abdu 'r-Rahman Chisti ametoa nukuu nyingi kutoka “Puran” zingine na hata katika “Ved”. Moja wapo ni hii iliyotafsiriwa hapa kutoka katika *Muqaddamah Tafsir Anwāru 'l-Qur 'ān*:-

- (a) Atharva Ved: Lailaha Harni Papan
Illallaha Paran Padam
Janm Baikunth Birap newti
to jane name Muhammadam.

Tafsiri: Kusema “Lailaha” huondoa dhambi
Kusema “Illa llah” huweka “Parm Padwi”
Kama unataka Pepo ya milele
Kila mara litaje jina “Muhammad”.

Atharva Ved ya sasa haina maneno hayo hapo juu. Lakini muasisi wa Arya Samaj Dyanand Saraswati amekubali katika kitabu chake, *Satyarth Parkash* (cha kiurdu) (Sura ya 14; uk. 739) kwamba Alloo Upnishad alitaja jina la Muhammad kuwa ni Rasul. Anaeleza kwamba mtu fulani, katika zama za Akbar (Mfalme wa Mughal) atakuwa ameliongeza katika Atharva Ved. Kisha anaandika: “Mtu anaweza kusema kwamba wawezaje kulidai wakati hakuna yeyote aliyelisema au kuliandika hivyo katika siku zote hizi? Tuna wezaje kukubali dai lako (la toleo la baadae) bila uthibitisho wowote? Lakini dai hili haliwezi kuwa ni la makosa kwa sababu tu yakuto kukubaliwa na yeyote”. Dai lililoje! Na uthibitisho ulioje!

AGANO LA KALE NA AGANO JIPYA

Sasa tunakuja katika vitabu vya ki-Yahudi na ki-Kristo. Kabla ya kutoa baadhi ya utabiri kutoka kwenye Biblia, jambo moja muhimu lazima liwekwe wazi kuanzia mwanzo.

Ni jambo la kawaida kwa Mayahudi na Wakristo kutafsiri hata majina halisi. Kwa hiyo popote watakopo likuta jina la “Muhammad”, wanalitafsiri kama “mwenye kusifiwa”, “mzuri” au maneno kama hayo. Tabia hii imewasaidia katika “kuficha ukweli” duniani, kwani watu wenye kusoma tafsiri hawawezi kamwe kushuku kuwa sentensi inamhusu mtu fulani. Sasa, ikiwa mwenendo huu utafuatwa na wengine, mtu asiyezungumza kiingereza atatafsiri jina “Livingstone” kama “Jiwe linaloishi” kisha atafafanua katika wazo hili na kujaribu kuonyesha kuwa katika karne ya 19, mawe yalikuwa na uhai huko Ulaya, na jiwe moja miongoni mwa mawe hayo lilikuja Afrika likasafiri hadi Kigoma na Ujiji nchini Tanzania.

Ongeza juu yake mabadiliko ya mara kwa mara na mageuzi ambayo Wakristo wanapendelea mno kuyafanya ndani ya Agano la Kale na Jipya, hapo ndipo unaweza kutambua hali halisi.

KITABU CHA MWANZO

Hata hivyo, hebu tuanzie kutoka kwenye kitabu cha

Mwanzo. Nitatumia tafsiri ya King James (Mfalme James) katika sehemu hii yote.

Mwanzo 17:20, inaelezea ahadi ya Mungu kwa Nabii Ibrahim: “Na kwa habari ya Ishmael, Nimekusikia: Nimembariki, nitamzidisha, nami nitamuongeza sana sana. Atazaa maseyid kumi na wawili, nami nitamfanya awe Taifa kuu.”

Dua inayokusudiwa ndani ya sentensi hii, imeelezwa kwa mapana na marefu sehemu nyingi ndani ya Qur’an, kama ifuatavyo:-

“Na (kumbukeni) Ibrahim na Ismail walipoiinua misingi ya Nyumba (wakaomba): Ee Mola wetu! Utukubalie, hakika Wewe ndiye Mwenye kusikia, Mwenye kujua.

“Ee Mola wetu! Wapelekee Mtume katika wao awesomee Aya zako na kuwafunza Kitabu na hekima na kuwatakasa. Hakika wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima.” (Qur’an, 2:127, 129)

KUMBUKUMBU LA TAWRATI

Mwenyezi Mungu alimuahidi Nabii Musa (a.s.).

“Mwenyezi Mungu, Mungu wenu atawateulieni nabii kutoka miongoni mwenu, miongoni wa ndugu zenu, kama nilivyo mimi; msikilizeni yeye.” (18:15).

“Mimi nitawaondokeshea nabii miongoni mwa ndugu zao mfano wako wewe, nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru. Hata itakuwa, mtu asiyesikiliza maneno yangu atakayosema yule kwa jina langu, nitalitaka kwake.” (18:18-19)

Wakristo wanajaribu kupachika utabiri huu kwa Nabii Isa (a.s.). Lakini haukubaliani na yeyote isipokuwa Mtume Muhammad Mustafa (s.a.w.w.) kwa sababu:-

1. Nabii (huyo) angekuja kutokana na ndugu wa (Bani) Israeli. Kwa hiyo Nabi yeyote atokanaye na Bani Israeli atakuwa hahusiki na habari hii njema. Sasa kama tujuavyo, Nabii Isa (a.s.) alitokana na Bani Israeli, ambapo Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alitokana na Bani Ismaili ambao walikuwa ni ndugu wa Bani Israel.
2. Nabii huyo atakuwa “mfano wa Musa”. Nabii Musa (a.s.) ilimbidi apigane vita, na Mtume Muhammad (s.a.w.w.) pia ilimbidi ajilinda kwa kupigana vita. Lakini Nabii Isa (a.s.) hakuwahi kamwe kuingia vitani.
3. Nabii Musa (a.s.) alikuwa na ndugu (yake) Haruna, ambaye alikuwa awe ndiye mrithi wake (baada ya kifo chake). Ndugu kama huyo hakuwepo kwa Nabii Isa (a.s.) ambapo Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alikuwa na Ali ibn Abi Talib (a.s.) aliyemwambia “wewe kwangu ni kama alivyokuwa Haruna kwa Musa, isipokuwa hakuna Nabii baada yangu”.

4. Nabii Musa (a.s.) aliacha uongozi wa kidini kwa wana wa Haruna. Nabii Isa (a.s.) hakufanya mpangilio kama huo. Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alifanya maandalizi kama hayo katika Ummah wake kwa kuacha Uislamu mikononi mwa Ali na wanae Hasani na Huseini (a.s.).
5. “.....nami nitatia maneno yangu kinywani mwake, naye atawaambia yote nitakayomwamuru.” Kigezo hiki kinamstahiki Mtume Muhammad (s.a.w.w.) pekee, kwani Nabii Isa (a.s.) hakudai hilo kwa ajili yake, wakati ambapo Allah (s.w.t.) alisema katika Qur’an kwa ajili ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.): “Wala hasemi kwa tamaa (ya nafsi yake). Hayakuwa haya ila ni Wahyi uliofunuliwa.” (Qur’an 53:3-4)
6. Nabii Isa (a.s.) hakuwahi kamwe kudai kuwa yeye ni Nabii aliyeahidiwa katika sentensi hii, wakati ambapo Allah (s.w.t.) alitaja kufanana huko baina ya Nabii Musa (a.s.) na Nabii Muhammad (s.a.w.w.) katika Qur’an katika Aya, “Hakika sisi tumekuleteeni Mtume aliye shahidi juu yenu, kama tulivyompeleka Mtume kwa Firaun.” (Qur’an 73:15)
7. Nabii Isa (a.s.) hakudai kuwa yeye ni mfano wa Musa (a.s.), wakati ambapo Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alimwambia Ali ibn Abi Talib (a.s.) “Wewe kwangu ni kama Haruna alivyokuwa kwa Musa, ispo kuwa hakuna Nabii baada yangu”.

8. Nabii Isa (a.s.) mwenyewe alisema kwamba Nabii ambaye angekuja baada yake ataukamilisha (atautimiza) utabiri huu. Angalia sentensi zifuatazo za Yohana:

“Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena” (Yohana 16:13).

TABIRI NYINGINEZO

(A) KUMBUKUMBU LA TAWRATI

“Akasema (yaani Musa), Bwana alitoka Sinai, Akawaondokea kutoka Seiri; Aliangaza katika kilima cha Parani na akaja na watakatifu elfu kumi. Upane wa mkono wake wa kuume Palikuwa na sheria ya moto-moto kwa ajili yao.” (Kumb. 33:2).

Kuja kwa Bwana kunamaanisha kuja kwa wawakilishi wa Mungu. Kwa hiyo Nabii wa Mungu aliyekuja kutokea Sinai alikuwa Nabii Musa (a.s.); na yule aliyeondoka kutoka Seiri (Mlima ulio Palestina) ni Nabii Isa (a.s.). Lakini ni Nabii yupi aliyeangaza kutoka Mlima Parani? Parani ni jina la Mlima uliopo Makkah. Nabii wa Mungu aliyeangaza kutokea huko si mwingine zaidi ya Muhammad Mustafa (s.a.w.w.).

(B) ISAYYAH

“Mwimbieni BWANA wimbo mpya, Na sifa zake tokea mwisho wa dunia;” (42:10)

Maradhi (matatizo) ya zamani ya kutafsiri majina ya halisi yameufanya utabiri huu usiwe na maana. Katika tafsiri ya ki-Armenia, iliyoandikwa mwaka 1666 na ikachapishwa mwaka 1733, (utabiri huo) umetafsiriwa kama ifuatavyo:- “Wanamuimbia Bwana wimbo mpya; na ufalme wake unaendelea baada yake; na jina lake ni Ahmad.” (Sasa jina la Ahmad limetafsiriwa kuwa lamaanisha ‘sifa zake’)

Vyovyote iwavyo, katika utabiri huu, wimbo mpya wa (kumuimbia) Bwana unamaanisha Sheria mpya kutoka kwa Mungu, (jambo ambalo) linafikiana (linakubaliana) na Mtume Mtukufu wa Uislamu; lakini haliwi hivyo kwa Nabii Isa (a.s.).

(C) HABAKKUK

Maono ya Nabii Habakkuk yanasema:

“Mungu alikuja kutoka Temani na Yeye aliy mtakatifu kutoka mlima Parani. Selah njia zake ni za milele” (3:3-6).

Naamini hakuna haja ya kuufasiri utabiri huu, ulio wazi sana. Mwakilishi wa Bwana aliyekuja kutoka Parani alikuwa ni Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na sifa nyingine zote zinaweza kutumika kwake kwa urahisi.

Allamah Fakhrul-Islam Muhammad Sadiq (aliyekuwa Padri wa kikristo hapo kabla) alifasiri (alisherehesha) zaidi ya tabiri 30 kutoka Agano la kale. Lakini kwa kuwa hiki ni kijitabu kifupi (kidogo), nimenukuu tu baadhi yake humu.

KUTOKA NDANI YA AGANO JIPYA

(A) “NABII YULE”

“Na huu ndio ushuhuda wake Yohana (yaani mbatizaji), Wayahudi walipotuma kwake makuhani na Walawi kutoka Yerusalemu ili wamwulize, Wewe u nani?”

“Naye alikiri, wala hakukana; alikiri kwamba, Mimi siye Kristo.

“Na Wakamwuliza, Ni nini basi? U Eliya wewe? Akasema, Mimi siye. Wewe u Nabii Yule? Akajibu, La” (Yohana 1:19-21).

Mazungumzo haya yanaonyesha wazi kwamba, kabla tu ya kuja Nabii Isa (a.s.) (Yesu Kristo), Mayahudi walikuwa wakisubiri Manabii watatu: Kristo, Eliya na ‘Nabii Yule’.

Na Yohana aliposema kuwa yeye si yeyote miongoni mwa wale watatu, kisha:

“Wakamwuliza, wakamwambia, Mbona basi wabatiza,

ikiwa wewe si Kristo, wala Eliya, wala Nabii Yule?”
(Yohana 1:25)

Inaonyesha vile vile kwamba “Nabii Yule” alikuwa na heshima kubwa hadi jina lake lilikuwa halitajwi, na sifa yake “Nabii” ikiandikwa kwa ‘N’ kubwa. Na kuja kwake kulikuwa kume-eleweka kiasi ya kwamba kumtaja tu kama ‘Nabii Yule’ kunatosha kumfahamu.

(B) “MSAIDIZI” (MFARIJI)

Nabii Isa (a.s.) amenukuliwa akiwaambia wanafunzi wake kumi na mbili:-

“ . . . yawafaa ninyi mimi niondoke, kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi (Mfariji) hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu. Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu. Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi; kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena; kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumwiwa.

“Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.

“Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa yaliyo yangu na kuwapasha habari.” (Yohana 16:7-14)

Marejeo mfano wa hizo zimetajwa katika Yohana 14:26 na 15:26.

Sidhani kuna haja ya kueleza ni vipi tabiri hizi zinakubaliana kikamilifu na Mtume Mtukufu wa Uislamu (s.a.w.w.).

Kuna zaidi ya tabiri thelathini zilizotajwa ndani ya *Anisu 'l-a 'laam*.

Sasa waweze kuelewa vema maana ya aya zifuatazo za Qur'an:

“Watu wa kitabu (ahlul-Kitab) wanamfahamu (yaani Muhammad (s.a.w.w.)) kama wanavyo wafahamu watoto wao; lakini baadhi yao wanauficha ukweli huku (wao wenyewe) wanaufahamu” (Qur'an, 2:146)

“Wale wanaomfuata huyo Mtume, Nabii asiyejua kusoma wala kuandika, ambaye wanamkuta ametajwa ndani ya Tawrati na Injili. . . ” (Qur'an, 7:157)

“Ingawa kutoka siku za zamani, wao (Mayahudi) walikuwa wakiomba ushindi dhidi ya wale bila imani, wakati alipowajia yule (yaani, Muhammad (s.a.w.w.)) ambaye walimfahamu, walikataa kumwamini yeye. . . .” (Qur'an, 2:89)

VITABU VYA KIPARSI (UMAJUSI)

Zarathustra, au Zoroasta, anatambulika kama mwanzilishi (muasisi) wa dini ya ki-Zoroasta (majusi), ambayo inafahamika kama U-Parsi (umajusi). Kuna aina mbiili za vitabu vya kiparsi: *Zend Avesta* na *Dasatir*.

Nanakili baadhi ya tabiri kutoka ndani ya kitabu cha A. H. Vidyarthi, *Muhammad in Parsi, Hindu and Buddhist Scriptures (Muhammad ndani ya vitabu vya kiparsi, kihindu na kibuddha)*:

Zend Avesta: Mungu alizungumza na Zoroasta kwa maneno yafuatayo: “Wenye nguvu zaidi miongoni mwa Maswahaba wa Waislamu, Ewe Zarathustra, ni wale watu wa sheria ya kale, au wale (watu) wa Soeshyant (ambao hawajazaliwa bado) ambao watairudisha dunia”. (Farvardin Yasht, XIII:17).

Dasatir: Ni mkusanyiko wa nyaraka 15 ambayo kwamba nyaraka wa Sasan I imeandika utabiri kuhusu Mtukufu Mtume wa Uislamu kwa maneno yaliyo wazi sana. Toleo hili la *Dasatir* lilichapishwa na Mulla Pheroze kwa msaada wa Makuhani wengine wengi wasomi wa kimajusi katika zama za Nasiru 'd-Din Shah Qachar wa Uajemi. Maandishi ya asili yamo katika lugha ya Ki-Pahlawi lakini kila sentensi inafuatwa na tafsiri yake ya Kiajemi ambayo ilifanyika bila shaka na Mulla Pheroze na timu yake ya makuhani.

Makusudio na kiini cha utabiri ni kwamba wamajusi wataiacha dini yao na watasambaratika:

“Watakapofanya matendo hayo, atadhihiri (atajitokeza) mtu miongoni mwa Waarabu ambaye kwamba mbele ya wafuasi wake, taji, kiti cha enzi, ufalme na dini (vyote) vitapinduliwa, na watu wenye kiburi watakomeshwa. Badala ya nyumba ya masanamu na hekali la moto, wataiangalia Nyumba ya Ibada ya Ibrahim bila ya kuwa na masanamu ndani yake na wataifanya kuwa Qibla chao.

“Na watakuwa ni rehema kwa walimwengu. Na kisha wataziteka Sehemu za mahekalu ya moto, na kuishinda Madain, Tus, Balkh, sehemu takatifu za wamajusi na maeneo yaliyo kando (yake). Nabii wao atakuwa ni mtu mwenye ufasaha, na ujumbe wake utakuwa ni wenye kushikamana barabara.”

ISBN 9987 620 20 5



Kimetolewa na Kuchapishwa na:
Bilal Muslim Mission of Tanzania
S.L.P. 20033
Dar es Salaam, Tanzaniaa